Cultural Orientation Resource Exchange



# Ajira kwa Wanawake Wakimbizi

Ajira nchini Marekani ni muhimu sana kwa maisha ya familia yako na ustawi wa baadaye, na pia maendeleo yako mwenyewe na uthabiti wa kifedha kama mwanamke. Watu wote wazima, wanaume na wanawake, wa umri wa kati ya miaka 18 na 64 na wanaoweza kufanya kazi, wanapaswa kuupa kipaumbele utafutaji ajira.

## MANUFAA YA KUFANYA KAZI



Wanawake na wanaume hufanya kazi nchini Marekani, na wanawake wanajumuisha idadi nusu ya wafanyakazi, hufanya kazi sawa na wanaume katika viwango vyote, na mara kwa mara huwasimamia wafanyakazi wa kiume. Kupata na kudumisha kazi kuna faida nyingi kwako wewe na familia yako.

**Kuisadia familia kumudu mahitaji –** Wakati wanandoa wote wawili wanafanya kazi, mapato ya familia huongezeka, hivyo kuwa rahisi kumudu gharama kama vile matumizi ya kila mwezi na kulipia kodi ya nyumba, na pia chakula na nguo. Mapato mara mbili pia hukuwezesha kuweka akiba ya pesa na kuongeza usalama wa kifedha familia yako.

**Kupokea manufaa –** Baadhi ya kazi zitajumuisha manufaa fulani kama vile bima ya afya ambapo mwajiri humlipia bima  mfanyakazi na mara nyingi kumlipa mapema sehemu ya malipo ya kila mwezi. Malipo yote ya bima hukatwa kwenye malipo ya mfanyakazi. Wamarekani wengi hutegemea mipango ya bima ya afya inayolipiwa na mwajiri kwa sababu huduma za afya zina gharama kubwa. Kupokea manufaa ya bima ya afya







kupitia mwajiri wako kunatoa huduma za afya mfululizo kwako wewe na familia yako kwa gharama ndogo.



**Kuboresha Kiingereza chako –** Kufanya kazi nje ya nyumbani kutakuwezesha kufanya mazoezi na kuboresha Kiingereza chako unaposhirikiana na wafanyakazi na wateja katika mazingira ya kitaaluma. Kujifunza Kiingereza kutakuwezesha kushiriki katika jamii yako na kuboresha uwezo wako wa kuendesha shughuli zako iwe unakwenda dukani, benki au kumwona daktari.

**Kushirikiana na wengine –** Mahali pa ajira panakupa nafasi ya kushirikiana na vikundi tofauti vya watu na kujua tamaduni na maadili ya Marekani, mambo ambayo yatakuwezesha kujijumuisha katika mazingira yako mapya.



**Kupata ujuzi wa kitaalamu –** Kazi yako ya kwanza itakupa ujuzi na ustadi wa kitaalamu ambao utakuandaa kwa kazi zako za baadaye. Jinsi unavyopata ujuzi zaidi ndivyo unavyopata nafasi kubwa zaidi ya kupandishwa cheo kazini au kupata kazi bora zaidi.





**Kutumia usafiri wa umma au kujifunza kuendesha gari –** Kusafiri kwenda na kutoka kazini kunaweza kukuhitaji utumie usafiri wa umma au kuendesha gari. Kujua jinsi ya kutumia usafiri wa umma au kuendesha gari kutachangia sana katika uhuru wako na kujitegemea, kukusaidia kujua mji wako na mahali unapoishi, na kukupa hisia ya kujumuika katika jamii yako mpya.


## KINA MAMA WAFANYAKAZI NA KINA MAMA AMBAO HAWAJAOLEWA



Wanawake wengi ambao huwalea watoto wao wadogo mara nyingi hukumbwa na ugumu wa kushughulikia mahitaji ya kazini na nyumbani kwa wakati mmoja, hasa ikiwa ni kina mama ambao hawajaolewa. Hata hivyo, kuna suluhisho za kuwasaidia kina mama wanaofanya kazi nje ya nyumbani.

Suluhisho moja ni kuwapeleka watoto katika vituo vya utunzaji wa mchana. Huduma za utunzaji wa mchana hulipishwa. *Early Head Start* ni mpango unaofadhiliwa na serikali kuu unaowahudumia watoto wa familia za mapato ya chini kutoka wakati wa kuzaliwa hadi umri wa miaka 3. Mpango mwingine, *Head Start* huzihudumia familia zilizo na watoto wa umri wa miaka 3 hadi 4. Kuandikisha watoto wadogo katika mojawapo ya mipango hii kutamwezesha mama ambaye hajaolewa, au wazazi wote wawili, kufanya kazi nje ya nyumbani. Suluhisho jingine ni kupata usaidizi wa marafiki, majirani au familia kama vile babu, nyanya na ndugu kama watoa huduma ya kuwatunza watoto ili kuwasaidia wazazi wanaofanya kazi. Kwa wanandoa, suluhisho la tatu ni kwa mmoja wa wazazi kutafuta kazi ya muda ya saa za jioni na wikendi, jambo ambalo litamwezesha mzazi mmoja kuwatunza watoto huku mzazi mwingine akiwa kazini.

## HALI ZA FAMILIA ZINAZOBADILIKA



Wamarekani wanathamini uhuru katika wanaume na wanawake. Katika familia nyingi, mume na mke wote hufanya kazi, na katika familia nyingine, mke hupata malipo zaidi kuliko mume. Katika familia zingine, mke amepata kazi na mume hana. Katika hali hii, mume atatarajiwa kuwatunza watoto wakati hawako shuleni.

Katika hali kama hizi, wanaume wengine wanaweza kuhisi kwamba wamepoteza nafasi yao ya uongozi katika familia. Wanawake wengine wanaweza kuhisi mfadhaiko wanapochukua majukumu mapya na kuwa walezi wakuu wanaokidhi mahitaji ya familia zao. Kusaidiana, pamoja na mawasiliano wazi na ya uaminifu, kunaweza kudumisha uelewa na kupunguza mafadhaiko kati ya mke na mume.

**Cultural Orientation Resource Exchange**

8719 Colesville Road, 3rd Floor ● Silver Spring, MD 20910

For more information, visit the CORE Resettlement Navigator website at **corenav.org**.

The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**